

MPITO: MWANZO MZURI WA SHULE

Karatasi ya habari kwa ajili ya familia

Kuanza shule kunaweza kuwa kugumu lakini pia wa kufurahisha. Karatasi hii ya habari inaelezea jinsi huduma ya chekechea ya mtoto wako ya mapema itasaidia mtoto wako kuwa na mwanzo mzuri wa shule.

Mtoto wako tayari amepitia hatua nyingi za mabadiliko, kama vile:

- kuhamza kutoka shughuli moja au utaratibu hadi nyingine
- kwenda kwa mchezo uliopangwa au likizo
- kuanzisha huduma ya watoto au shule ya chekechea.

Uzoefu huu unakupa wazo la jinsi mtoto wako anavyoitikia maeneo mapya na vitu, na msaada anaohitaji.

KWA NINI MWANZO MZURI WA SHULE NI MUHIMU?

Mwanzo mzuri wa shule humsaidia mtoto wako:

- kufikia matokeo bora ya mafunzo na ustawi
- kuepuka usumbu kwa masomo na maendeleo yake
- kujihisi salama, kujiamini na kushikamana.

KUANDIKISHA MTOTO WAKO SHULENI

Shule nyingi zinaanza uandikishaji mwezi Mei mwakani kabla ya watoto kuanza shule. Kuandikisha kunakupa fursa zaidi za kujua shule na kushiriki katika mpito kwa shughuli za shule. Watoto hubadilika vizuri wakati shughuli hizi zinapoanza vizuri kabla ya mwisho wa mwaka na kuendelea baada ya siku chache za kwanza za shule.

MPITO KWA MIPANGO NA SHUGHULI ZA SHULE

Mpito wa shughuli za shule hukusaidia wewe na mtoto wako:

- kuelewa shule itakuwaje
- kutafuta marafiki na watoto wengine na familia.

TAARIFA YA MAFUNZO YA MPITO NA MAENDELEO

Mwalimu wa chekechea wa mtoto wako ataandika Taarifa ya Mafunzo ya Mpito na Maendeleo (inayojulikana kama Taarifa ya Mpito). Taarifa ya Mpito husaidia shule ya mtoto wako na mwali muwa maandalizi kupata kujua mtoto wako na kupanga masomo yake. Taarifa ya Mpito itajumuisha:

- jina la mtoto wako, tarehe ya kuzaliwa na picha
- jina lako na maelezo ya mawasiliano
- jina na maelezo ya mawasiliano ya huduma ya chekechea na wataalamu wengine wa mapema wa utotoni ambao wanasaidia mtoto wako
- habari kuhusu maslahi ya mtoto wako, ujuzi na uwemo
- mikakati bora ya kufundisha mtoto wako.

Ikiwa mtoto wako atakwenda kwenye Utunzaji wa Nje ya Saa za Shule (OSHC), Taarifa ya Mpito inashirikiwa na huduma ya OSHC pia.

Utapewa nakala ya Taarifa ya Mpito ya mtoto wako iliyokamilika. Inaweza kukusaidia kuelewa, kusaidia na kujadili masomo ya mtoto wako.

Taarifa ya Mpito ya mtoto wako husaidia:

- kupanga maslahi ya mtoto wako
- kusaidia mabadiliko mwanana kutoka kwa huduma ya chekechea ya mtoto wako hadi shuleni.

Taarifa za Mpito kwa kawaada huandikwa katika Muhula wa 4. Hata hivyo, ikiwa mtoto wako ana ulemavu au ucheleweshaji wa ukuaji, Taarifa ya Mpito inaweza kuandikwa mapema, mwezi Juni au Julai. Hii hukusaidia wewe na shule kuanza kupanga msaada wowote wa ziada wa mtoto wako.

Taarifa ya Mpito ina sehemu unayohitaji kujaza. Kwa sababu unaaja mengi kuhusu mtoto wako, mawazo yako ni ya thamani. Itasaidia shule kupanga mwanzo mzuri wa shule kwako na mtoto wako.

Pia kuna sehemu ya mtoto wako kujaza, akisaidiwa na mtu mzima kama wewe au mwali muwa wake wa chekechea. Inaweza kujumuisha:

- mchoro
- kile ambacho mtoto wako anapendelea kuhusu shule
- anachofikiria kuhusu kuanza shule.

JINSI HABARI INAVYOSHIRIKIWA

Taarifa za Mpito zinashirikiwa na kuhifadhiwa mtandaoni kwa kutumia Insight Assessment Platform. Maeleo kuhusu Insight Assessment Platform yanahifadhiwa salama nchini Australia.

Shule zote za serikali ya Victoria (na baadhi ya shule za Kikatoliki na za Kujitegemea) hutumia Insight Assessment Platform kurekodi mafunzo na maendeleo ya kila mtoto. Ikiwa shule ya mtoto wako haitumii Insight Assessment Platform, atapewa karatasi au nakala ya elektroniki ya Taarifa ya Mpito.

Idara ya Elimu na Mafunzo wakati mwingine hutumia watoa huduma za nje. Watoa huduma wanaofanya kazi katika Idara lazima watumie hatua za usalama wa habari. Insight Assessment Platform linakubaliana na Idara **Sera ya Faragha ya Taarifa** www.education.vic.gov.au/Pages/privacypolicy.

Idara inaweza kutumia taarifa kutoka kwa Taarifa za Mpito kwa ajili ya ufuutilaji na utafiti. Habari hii itawasilishwa kwa idadi na grafu na watoto **hawataweza** kutajwa

Kwa maeleo zaidi kuhusu Insight Assessment Platform, wasiliana na Idara kwenye psts@edumail.vic.gov.au.

Wakati mwingine elimu ya Victoria na wataalamu wa utunzaji wanahitaji kushiriki habari ili kukuza ustawi wa mtoto au usalama. Huduma yako ya elimu ya chekechea inaweza kushiriki habari kuhusu mtoto wako na familia pale inapohitajika ili kutimiza wajibu wake wa utunzaji, kupambana na ubaguzi, afya na usalama wa kazi, na majukumu ya ustawi wa mtoto na usalama. Kwa habari zaidi tembelea, <https://www.vic.gov.au/information-sharing-schemes-and-the-maram-framework>.

KWA HABARI ZAIDI

Tafadhalii tembelea

www.education.vic.gov.au/transitiontoschool

Waraka huu unapatikana katika lugha tofauti kwa

www.education.vic.gov.au/transitiontoschool